


Chanjo Familia Inaweza Kuamini	"Vaccines Families Can Trust" was created and translated October 20, 2023 by the Multilingual Health Education Alliance (M-HEAL). [Swahili]	
	Iyi karatasi inaendeya kwa mapendekezo ya <u>ma ofisi ya kufuatiliya magonjwa na kujikinga</u> mu Amerika kuanzia tarehe 10, Februari 2023.	
Upimaji katika Laboratoire	Wanasayansi wanatumia miaka mingi kupima chanjo kwenye laboratory ili waone kama inaweza kumkinga mtu kutokana na ugonjwa fulani.  Kama matokeo ya bipimo yanaonekana kuwa mazuri <b>Usimamizi wa Chakula na Dawa (FDA) mu inchi Amerikani</b> inaweza kuitika kupima na watu.	
Hatua ya 1 Kupima na Watu: Usalama & Dozi	Wakati ya hatua ya kwanza ya kupima na watu 20-100 walijitolea, wanasayansi watajifunza usalama wa chanjo na matokeo mabaya yayo. Watamua pia kipimo cya dozi ya chanjo inashahili.	
Hatua ya 2 Kupima na Watu: Matokeo mabaya & Mwitikio wa Kinga	Wakati ya hatua ya pili ya kupima na mamia ya watu waliojitolea, wanasayansi walijifunza ni matatizo gani yanayojulikana zaidi. Wanangalia pia mwitikio ya mwili kwa chanjo ili wahakikishe ya kwamba ina nguvu ya kutosha kuzuia ugonjwa io.	
Hatua ya 3 Kupima na Watu: Faida	Wakati ya hatua ya tatu ya kupima na maelfu ya watu waliojitolea, wanasayansi wanalinganisha jinsi chanjo hiyo inavyolinda watu wanaopokea chanjo ile ikilinganishwa na watu ambao hawapati. Wanasayansi pia watatafuta zaidi kama kuko matokeo mabaya yoyote na matatizo yoyote ya usalama wa chanjo.	
Kama chanjo inafanikiwa katika hatua zote tatu, FDA ita angalia data zote za kisayansi ili kuzingatia kuitika chanjo hiyo kwa matumizi ya watu.		
FDA inaitika chanjo KAMA:	<ul style="list-style-type: none"><li>• Iko salama na inafanya kazi</li><li>• Faida ni kubwa kuliko hatari</li><li>• Mtengenezaji wa chanjo ilienesha kanuni za usalama</li></ul>	
Nyumba za utengenezaji ya chanjo zinahitajika kufanyiwa ukaguzi ya usalama na ubora ya FDA wakati yote ya utengenezaji wa Chanjo		
Madaktari na wataalam wengine watatoa mapendekezo ya kutumia chanjo	Komite ya Ushauri ya Mbinu za Chanjo (ACIP) waliaangalia data zote za kisayansi kuhusu chanjo. Wanatoa pendekezo kwa CDC ikiwa itaitumia ao kutokutumia na nani (watoto, kwa mfano) wanapaswa kuipata. Kisha Mkurugenzi wa CDC ataamua kama chanjo itaongezwa kwenye ratiba ya chanjo ya Amerika.	
Baada ya iyo, chanjo inafuatiliwa kila wakati kwa usalama.		
<ul style="list-style-type: none"><li>• Nyumba za kutengeneza chanjo zitaendelea kufanyiwa ukaguzi ya usalama na ubora ya FDA</li><li>• Mutu yoyote anaweza kuwasilisha ripoti kwa CDC kuhusu tatizo kubwa la kiafya alilopata baada ya chanjo</li><li>• Wanasayansi wanatumia data ya matibabu kutoka kwa mamilioni ya watu ili waendeleo kutafuta matatizo ya usalama ya chanjo</li><li>• Kama chanjo itapatikana kuwa sio salama, FDA na CDC itasimasha ruhusa, na chanjo haiwezi tena kutolewa mu inchi Amerikani.</li></ul>		